# TAARIFA YA HALI MBAYA YA HEWA KWA MWEZI SEPTEMBA NA OKTOBA, 2023

## 1.0 UTANGULIZI

Katika kipindi cha mwezi Septemba 2023 hali ya ukavu iliendelea kujitokeza katika maeneo mengi ya nchi ikiambatana na hali ya joto. Aidha, kwa mwezi Oktoba, 2023 ongezeko kidogo la mvua lilijitokeza katika baadhi ya maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka ikiashiria kuanza kwa msimu wa mvua za Vuli, 2023. Hali hii ilisababisha ongezeko kidogo la unyevu ardhini, kina cha maji na malisho kwa maeneo machache. Hata hivyo, vipindi vya upepo mkali vilijitokeza katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa pwani, kati mwa nchi, nyanda za juu kusini magharibi na maeneo ya maziwa makuu. Hali ya hewa iliyojitokeza pamoja na athari zake imeendana na taarifa ya mwelekeo wa mvua za Vuli (Oktoba-Disemba), 2023.

### 1.1 Mvua kubwa kwa mwezi Septemba, 2023

Katika kipindi cha mwezi Septemba 2023, vipindi vya mvua vilijitokeza katika maeneo machache, hususan ukanda wa pwani, ziwa Victoria na nyanda za juu kaskazini mashariki. Aidha, katika kipindi hiki vipindi vichache vya mvua kubwa vilivyojitokeza nchini. Mnamo tarehe 11 Septemba, 2023 kituo cha Bukoba (Mkoa wa Kagera) kilipima milimita 50.3 za mvua.

### 1.2 Hali joto kwa mwezi Septemba, 2023

Katika kipindi cha mwezi Septemba, 2023 maeneo machache ya nyanda za juu kusini magharibi yaliendelea kupata vipindi vya baridi ukilinganisha na maeneo mengine ya nchi. Kiwango kidogo zaidi cha joto la chini cha nyuzi joto 7.5 °C kilirekodiwa katika kituo cha Uyole mkoani Mbeya mnamo tarehe 1 Septemba, 2023. Kwa ujumla maeneo ya Uyole na Igeri yaliendelea kuwa na hali ya baridi ambapo viwango vya joto la chini vilishuka zaidi ya nyuzi joto 10 °C.


Kielelezo cha 1 kinaonesha viwango vya joto la chini kwa siku katika mwezi Septemba, 2023 kwa vituo vya Uyole na Igeri. Kwa ujumla, hali ya baridi iliendelea kujitokeza katika wiki ya kwanza ya Septemba ikifuatiwa na ongezeko kidogo la joto katika wiki ya pilikuelekea mwishoni mwa mwezi. Hata hivyo, viwango vya joto la chini vinaonesha vipindi vya baridi vilijitokeza zaidi katika maeneo ya Igeri ambapo kwa siku 20 ndani ya mwezi kiwango cha joto kilikuwa nyuzi 10 °C au chini zaidi.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610

Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

*728G _ 01/2023*




**Kielelzo 1.** Viwango vya joto la chini katika kituo cha Uyole na Igeri kwa mwezi Septemba, 2023.

Kwa upande wa viwango vya juu vya joto, hali ya joto zaidi ilijitokeza katika baadhi ya maeneo hususan magharibi mwa nchi na ukanda wa ziwa Victoria. Kiwango cha juu zaidi cha nyuzi joto 35.2 °C kilirekodiwa katika kituo cha Mpanda kilichopo mkoani Katavi mnamo tarehe 29 Septema, 2023 ikifuatiwa na Ibadakuli (Shinyanga) na mpanda, vyote vilirekodi nyuzi joto 35 °C mnamo tarhe 30 na 17 Septemba, 2023 mtawalia.

### 1.3 Upepo Mkali kwa mwezi Septemba, 2023

Katika mwezi huu, vipindi vya upepo mkali unaofika kilomita 40 hadi 50 kwa saa na baadhi ya nyakati kufikia kilomita 60 kwa saa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini yakiwemo ya ukanda wa pwani (Mikoa ya Tanga, Dar es Salaam, Lindi, Mtwara pamoja na Visiwa vya Unguja na Pemba). Aidha, maeneo ya kati mwa nchi (Singida na Dodoma), magharibi (Tabora), nyanda za juu kusini magharibi (Songwe) pamoja na maziwa makuu pia yaliathiriwa na vipindi vya upepo mkali. Kasi na nguvu ya upepo ilisababisha athari mbalimbali ikiwemo ongezeko la vumbi, kupeperusha takataka na kusabisha kupungua kwa uono. Maeneo ya mwambao wa pwani yalipatwa na vipindi vya mawimbi makubwa ya bahari na kuathiri baadhi ya shughuli zinazofanyika baharini sambamba na kuhatarisha jamii zinazofanya shughuli mbalimbali katika mwambao.


### 1.4 Mvua kubwa kwa mwezi Oktoba, 2023

Katika kipindi cha mwezi Oktoba, 2023 vipindi vya mvua vilivyoashiria kuanza kwa msimu wa mvua za Vuli, 2023 vilijitokeza katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa pwani ya kaskazini, ziwa Victoria na nyanda za juu kaskazini mashariki. Aidha, vipindi

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610

Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

vichache vya mvua kubwa vilijitokeza katika maeneo mbalimbali ya nchi. Mnamo tarehe 30 Oktoba, 2023 kituo cha Mlingano kilichopo mkoani Tanga kilipima milimita 92.1 za mvua kwa saa 24 ikiwa ni kiwango cha juu zaidi kwa mwezi Oktoba, 2023 ikifuatiwa na Bukoba (milimita 57.1) tarehe 17 Oktoba na Matangatuani (milimita 56.2) mnamo tarehe 19 Oktoba,2023. Vituo vilivyoripoti vipindi vya mvua kubwa vya milimita 50 au zaidi ni kama vinavyoonekana kwenye Kielelezo 2. Ripoti kutoka katika vyombo vya habari zilithibitisha kutokea kwa mvua kubwa iliyosababisha athari katika baadhi ya maeneo ya wilaya ya Bukoba (Kielelezo 2).




**Kielelezo 2:** Viwango vya mvua kubwa kwa mwezi Oktoba, 2023



**Kielelezo 3**. Majengo yaliyoezuliwa paa baada ya mvua kubwa kunyesha ikiambatana na upepo mkali Bukoba (*Chanzo: gazeti la Habari Leo*).

**1.5 Hali joto kwa mwezi Oktoba, 2023**

Katika kipindi cha mwezi Oktoba 2023, vipindi vichache vya baridi vilijitokeza kwa nyakati za usiku hususan katika mikoa ya Mbeya na Njombe. Kiwango cha chini zaidi cha nyuzi joto 7.4°C kiliripotiwa katika kituo cha Uyole (Mkoa wa Mbeya) mnamo tarehe 4 Oktoba, 2023. Kwa upande wa viwango vya juu vya joto, baadhi ya maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi (Mkoa wa Songwe), magharibi (Mpanda, Tabora na Kigoma) na ukanda wa ziwa Victoria (Ibadakuli (Shinyanga)) yalirekodi viwango vikubwa vya joto la juu. Kiwango cha juu zaidi cha nyuzi joto 36.7 kilirikodiwa katika kituo cha Songwe mnamo tarehe 13 Oktoba, 2023. Aidha, Hali ya joto ilijitokeza zaidi Mpanda (mkoa wa Katavi) ambapo kwa siku 12 viwango vya joto la juu vilikuwa nyuzi joto 35°C au zaidi.

**Jedwali 1**. Idadi ya siku ambazo viwango vikubwa vya joto la juu vilijitokeza kwa mwezi Oktoba, 2023

| Kanda | Kituo | Siku | Kiwango cha Joto la Juu ($^0$C) |
|---|---|---|---|
| Nyanda za Juu Kusini Magharibi | Songwe | 2 | ≥ 35 °C |
| Magharibi | Mpanda | 12 | ≥ 35 °C |
| | Tabora | 7 | ≥ 35 °C |
| | Kigoma | 1 | ≥ 35 °C |
| Ukanda wa Ziwa Victoria | Ibadakuli | 6 | ≥ 35 °C |

**1.6 Upepo Mkali kwa mwezi Oktoba, 2023**

Katika kipindi cha mwezi Oktoba, vipindi vya upepo mkali unaofika kilomita 40 hadi 50 kwa saa, na baadhi ya nyakati kufikia kilomita 60 kwa saa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini ikiwemo ukanda wa pwani (Mikoa ya Tanga, Dar es Salaam, Lindi, Mtwara pamoja na Visiwa vya Unguja na Pemba) hususan wiki ya nne ya mwezi. Aidha, maeneo ya kati mwa nchi (Singida na Dodoma), magharibi (Tabora), nyanda za juu kusini magharibi (Songwe) pamoja na maziwa makuu pia yaliathiriwa na vipindi vya upepo mkali. Nguvu ya upepo mkali ilisababisha athari mbalimbali katika maeneo hayo.

*Matukio haya ya hali mbaya ya hewa yanaonesha ongezeko la changamoto zinazosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi na umuhimu wa kutekeleza mikakati thabiti ya kukabiliana mabadiliko hayo ili kulinda jamii na mazingira*.

*Imetolewa: tarehe 16 Novemba, 2023*
**Na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610

Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

*728G _ 01/2023*